# HALMASHAURI YA MJI KONDOA

## HABARI ZA WIKI

TOLEO NA:4

JUMATATU, FEB 20-FEB 26, 2023


KONGAMANO LA FURSA



## Vijana Kondoa Mji watakiwa kuchangamkia fursa kujiinua kiuchumi

Na. Sekela Mwasubila, Mji Kondoa

Vijana katika Halmashauri ya Mji Kondoa wametakiwa kuchangamkia fursa mbalimbali za kuwaingizia kipato zinazopatikana katika Halmashauri ya Mji ili waweze kujiinua kiuchumi na kuondokana na utegemezi.

Ushauri huo ulitolewa na Mbunge wa Jimbo la Kondoa Mjini Mhe. Juma Makoa akiwa mgeni rasmi katika kongamano la kutangaza fursa mbalimbali kwa wajasiriamali wa Halmashauri ya Mji Kondoa lililoandaliwa na Divisheni ya Maendeleo ya Jamii na kufanyika katika ukumbi wa Kondoa Irangi hivi karibuni.

“Fursa Kondoa zimeonekana ni nyingi mno na kwasasa tumefunguka kiutalii zaidi ya watalii 5000 wanakuja kwenye kituo cha michoro mapangoni kwa mwaka lakini hakuna mtu hata mmoja anayejishughulisha Kolo wengi ni wageni kutoka maeneo mengine tuamke kama meneja alivyoelezea , tumefungua Mkungunero na inafikika, bonde la Swagaswaga serikali imejenga miundombinu fursa nyingi zipo ila bahati mbaya jinsi ya kuzifikia ndio hatujui,”amesema Mhe. Makoa

YALIYOMO NDANI


NUKUU MBALIMBALI ZA WADAU

MALENGO YA KONGAMANO UK. 3

MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA UK. 4

MKULIMA KUTOKA KONDOA UK. 5

MENEJA WA TARURA KONDOA UK. 6

MENEJA MICHORO MAPANGONI KOLO UK. 7

MWAKILISHI WA WATU WENYE ULEMAVU UK. 8

PICHA UGAAJI WA MITI YA MATUNDA UK 9

MATUKIO MBALIMBALI STENDI YA BICHA UK 10

## KONGAMANO LA FURSA



INATOKA UK 1

# Vijana Kondoa Mji watakiwa kuchangamkia fursa kujiinua kiuchumi

Aidha aliongeza kuwa serikali imeleta miradi katika kila kata ikiwemo ujenzi wa Zahanati, Vituo vya Afya na madarasa lakini vibarua na mafundi wanaotumika katika kazi hizo ni kutoka nje ya Halmashauri ya Mji jambo ambalo si sahihi kwa kuwa lengo la serikali pia ni kupunguza umaskini kwa wananchi wa eneo husika.

“Kulikuwa na vijana walichukuliwa kwa ajili ya kazi ya kuchimba mitaro ya maji walikimbia na hawajui kazi za Serikali zina muda maalum na zinatakiwa zikamilike kwa muda huo Mkanadarasi kweli achukue watu kutoka Songea na vijana wetu wapo hapa tuambiane tu ukweli vijana wetu ni wavivu hawataki kuchangamkia fursa,”amesisitiza Mhe. Makoa.

Aidha aliwapongeza wanawake wengi waliojitokeza katika kongamano hilo na kusikitishwa na vijana na wanaume kubaki nyuma kushiriki kwenye makongamano kama hayo ambayo yanawafungulia fursa mbalimbali ambazo zitawaongezea kipato na kuwainua kiuchumi na hivyo amewataka wazazi kuendelea kuzungumza na vijana kwa kuwaambia ukweli kuwa waache uvivu.

Akitoa mada wakati wa kongamano hilo Meneja wa kituo cha Michoro ya Mapangoni Kolo Ndg. Zuberi Mabie aliwashauri wananchi wa Kolo na Halmashauri ya Mji kwa ujumla kutumia fursa za utalii zilizopo katika kituo hicho ambazo kwasasa zinafanywa na watu kutoka sehemu nyingine.

“Fursa zilizopo Kolo kituoni pale ni nyingi ambazo ni malazi kwa wageni, ngoma za asili, kuongoza wageni kwenye mapango yenye michoro, usafirishaji wa watalii, kuanzisha maduka ya zawadi kwa wageni, kufuma na kushona vikoi, kuanzisha kampuni za kitalii na utoaji wa huduma za kifedha kwa kuwa wageni wengi wanakuja na kadi za benki za nje,”amesema Meneja Zuberi

Akitoa ushuhuda kwa niaba ya wanufaika wa mikopo ya asilimia 10 katika Halmashauri ya Mji Kondoa Bi. Hawa Hassan aliishukuru serikali kwa kuwapatia mikopo kwa kuwa imebadilisha kwa kiasi kikubwa maisha yao na wameondokana na hali ya utegemezi kama ilivyokuwa awali.

Mafunzo ya kuwajengea uwezo wajasiriamali na kuwapatia fursa zinzopatikana katika taasis mbalimbali limefanyika ambapo wataalam kutoka TARURA, Ardhi, Michoro ya Mapangoni na Kilimo walitoa mada za kuonyesha fursa mbalimbali katika taasis hizo na limehudhuriwa pia na baadhi ya Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Mji Kondoa.

## KONGAMANO LA FURSA




**Irene Mosha**
**Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii**
**Halmashauri ya Mji Kondoa**

### MALENGO YA KONGAMANO LA FURSA ZA KIUCHUMI LILILOANDALIWA NA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII KATIKA HALMASHAURI YA MJI KONDOA

- **Kutambua na kuzitumia fursa za kiuchumi zilizopo katika Halmashauri ya Mji Kondoa kwa wajasiriamali, vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu**
- **Kubadilishana mawazo na uzoefu wa kibiashara kwa Wajasiriamali, vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu**
- **Kuwawezesha Wajasiriamali waweze kukua kutoka kwenye ujasiriamali mdogo kwenda kwenye ujasiriamali wa kati**
- **Kutengeneza mtandao (networking) wa kibiashara kwa wadau wote wa biashara, mitaji na masoko**
- **Kugawa miti ya matunda kwa Wajasiriamali, vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ili kuendeleza juhudi za Serikali za utunzaji wa Mazingira**

# NUKUU ILIYOTOLEWA NA MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA KATIKA KONGAMANO LA FURSA ZA KIUCHUMI ZILIZOPO KATIKA HALMASHAURI YA MJI KONDOA



"Katika eneo letu suala la vijana kujituma bado halijakaa vizuri wanapaswa kujishughulisha hakuna sababu ya vijana kukaa bila kazi wakati fedha za mikopo zipo tena isiyo la riba na hakuna urasimu. Pia vijana tunawaomba mchangamke kujitolea nguvu kazi katika kazi mbalimbali zinazoendelea kutoka Serikali, wazazi tuna kazi kubwa ya kwenda kuwajengea uwezo vijana wetu kuwa kazi zipo hivyo wasichague kazi za kufanya kwa anayetaka fursa atazipata endapo tu tukikubaliana na masharti yake."

**Mhe. Mohamed Abdi Kiberenge**
**MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA**

# NUKUU ILIYOTOLEWA NA MTAALAM WA KILIMO KATIKA KONGAMANO LA FURSA ZA KIUCHUMI ZILIZOPO KATIKA HALMASHAURI YA MJI KONDOA



"Kama tukiweka imani katika kufanikiwa basi tutafanikiwa kweli, wengi wetu hapa tunadhani kuwa na shamba kubwa ndio kupata mavuno mengi na ndio kufanikiwa si kweli unaweza kuwa na eneo dogo na bado ukafanikiwa kwani utajili wa kweli ni ule unaokuja polepole.
Zitumieni fursa zilizopo ni nyingi sana ambazo mnaweza kuanza kwa mitaji hiyo hiyo midogo midogo kama kilimo cha mahindi, alizeti, vitunguu, ufugaji wa mbuzi, ng'ombe wa maziwa na ufugaji wa kuku wa mayai na nyama."

Iteo Yohana
Mtaalam wa Kilimo
Kanisa Katoliki Jimbo la Kondoa

# NUKUU IILIYOTOLEWA NA KAIMU MENEJA KUTOKA TARURA KONDOA KATIKA KONGAMANO LA FURSA ZA KIUCHUMI ZILIZOPO KATIKA HALMASHAURI YA MJI KONDOA



"Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) wametenga fedha zaidi ya milioni 300 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za barabara kama kufanya usafi wa barabara, lakini nasikitika sijaona vikundi ambavyo vimeomba hadi sasa kufanya kazi hiyo kutoka Kondoa. Naomba niwashauri jiungeni kwenye vikundi mvisajili halafu mtasajiliwa tena PPRA na si lazima uwe na mtaji mkubwa tumeacha fursa wanatumia wengine tuamke na kutumia fursa zilizopo katika sekta ya barabara."

Mhandisi William Tigahwa
TARURA KONDOA

# NUKUU ILIYOTOLEWA NAMENEJA WA KITUO CHA MICHORO MAPANGONI KOLO KATIKA KONGAMANO LA FURSA ZA KIUCHUMI ZILIZOPO KATIKA HALMASHAURI YA MJI KONDOA



"Katika mapango yaliyopo Kolo fursa zipo nyingi ikiwemo malazi kwa wageni, usafiri kwa wageni kwenda mapangoni, kufungua maduka ya zawadi, vikundi vya ngoma, kufuma, kushona na ufinyanzi, kuanzisha kampuni za kitalii na kuanzisha huduma za kifedha.Fursa hizi kwasasa wanafanya wageni wanaotoka nje ya Kondoa.

Aidha nawashauri wakazi wa Kondoa na maeneo mengine mtenge muda wa kutembelea katika maeneo ya vivutio kama Kolo wa ajili ya kumwagilia moyo na kupumzisha akili."

Zuber Mabie
Mneneja Kituo cha Michoro Mapangoni Kolo

# NUKUU ILIYOTOLEWA NA MWAKILISHI WA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA KONGAMANO LA FURSA ZA KIUCHUMI ZILIZOPO KATIKA HALMASHAURI YA MJI KONDOA



Tunaomba tuchukue nafasi hii kuishukuru Serikali inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuwezesha walemavu kupata mikopo isiyo na riba na kuruhusu mikopo kutolewa hata kwa mtu mmoja.

Aidha tunawaomba wenzetu wengine wenye ulemavu watumie fursa hii kupata mikopo na kujiinua kiuchumi kwani wengi wameshanufaika na mikopo hii hapo awali na utaratibu wa kujiunga nendeni kwenye ofisi za Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri ya Mji Kondoa kila kitu mtaelekezwa.

Mzee Abedi Abubakari Duttu
Mwakilishi wa vikundi vya Watu wenye ulemavu

# MITI 100 YA MATUNDA ILITOLEWA NA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII KWA WALIOHUDHURIA KATIKA KONGAMANO LA FURSA ZA KIUCHUMI ZILIZOPO KATIKA HALMASHAURI YA MJI KONDOA IKIWA NI KUUNGA MKONO KAMPENI YA LISHE













# MATUKIO MBALIMBALIKATIKA STENDI MPYA YA MABASI BICHA







*Zoezi la uletaji wa huduma ya umeme katika Stendi Mpya ya Mabasi Bicha limefanyika na Shirika la Umeme Tanzania. Picha kushoto ni Mkurugenzi wa* ***Halmashauri ya Mji Kondoa Paul Mamba Sweya*** *akichimba shimo kwa ajili ya kuweka nguzo ya umeme.*



Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Umwagiliaji Halmashauri ya Mji Kondoa Ndg. Hassan Kiseto(aliyenyoosha mkono)akitoa maelekezo kwa wafanyabiashara waliomba kujenga vibanda katika Stendi Mpya ya Mabasi Bicha.



Mkuu Kitengo cha Huduma za Sheria Halmashauri ya Mji Kondoa Ndg. Shaban Sued (aliyenyoosha mkono)akitoa maelekezo ya ugawaji viwanja kwa wafanyabiashara waliomba kujenga vibanda katika Stendi Mpya ya Mabasi Bicha.